

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WIZARA YA AFYA

### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MWENENDO WA UGONJWA WA MARBURG, WILAYA YA BUKOBA VIJIJINI, MKOANI KAGERA

**Dar es Salaam, 04 Aprili, 2023.**

**Ndugu Wananchi**, mtakumbuka kuwa mnamo tarehe 21 Machi, 2023 Wizara Afya ilitoa Taarifa kwa umma juu ya Ugonjwa wa Marburg katika Wilaya ya Bukoba vijijini, mkoani Kagera. Napenda kuwafahamisha kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na jamii yote tumeendelea kuchukua hatua za kukabiliana na kudhibiti ugonjwa huu tangu ulipotangazwa. Nashukuru kwamba jitihada hizi zimezaa matunda na ugonjwa haujasambaa zaidi ya kata mbili za Bukoba Vijijini zilizoathirika.

**Ndugu Wananchi**, Hadi kufikia leo tarehe 4 April 2023, jumla ya visa ni 8 na kati yao watu 5 wamefariki. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa, **hatujapata wagonjwa wapya, wala vifo**. Aidha ninayo furaha kubwa kuwajulisha kuwa **leo tumemruhusu mgonjwa mmoja mwanaume mwenye umri wa miaka 26 akiwa na afya njema**. Ni matumaini yangu kuwa jamii itampokea vyema na kushirikiana nae katika shughuli zake za kila siku. Wagonjwa wawili (2) waliolazwa wanaendelea vizuri na matibabu katika vituo maalum vilivyoandaliwa. Serikali inatoa shukrani za pekee kwa wataalam wote wa afya walioko mstari wa mbele kwa kutoa huduma bora kwa wagonjwa wetu usiku na mchana bila kuchoka.

**Ndugu Wananchi**, hadi kufikia tarehe 04 Aprili, 2023 jumla ya watu 212 waliotangamana na wagonjwa wamebainishwa. Kati ya hawa, watu 35 wamemaliza siku 21 za uangalizi bila kuonesha dalili zozote za ugonjwa huu na hivyo tumewaruhusu kutoka katika karantini na kurejea kwenye familia na shughuli zao. Hii ni ishara nzuri sana kwetu, Wizara ya Afya, Serikali na Taifa kwa ujumla kwa kuwa maambukizi ya Virusi vya Marburg nchini yamedhibitiwa kwa wakati.

**Ndugu Wananchi**, Serikali bado inahimiza wananchi wote na hasa wa Mkoa wa Kagera kuendelea kuchukua tahadhari, kudhibiti ugonjwa na kuzuia maambukizi mapya katika jamii. Nisisitize tena kwamba, endapo kutakuwa na mtu yeyote kwenye jamii mwenye dalili za homa kali, kutapika, kuharisha, kutoka damu na mwili kuishiwa nguvu, tutoe taarifa haraka kwa kupiga simu 199 bila gharama ili kupata msaada wa wataalam haraka na kuchukua hatua zinazostahili. Pia tuepuke kumgusa mgonjwa au majimaji ya mwili wake ikiwemo mate, machozi, damu, mkojo, kinyesi pamoja na matandiko na nguo za mgonjwa bila kinga. Aidha, tuendeleo kuzingatia unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuosha matunda na kula chakula kilichopikwa kikamilifu.

**Ndugu Wananchi**, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), hata pale mgonjwa wa mwisho kupona atakaporuhusiwa, hatuna budi kuendelea kuchukua tahadhari hadi tutakapojiridhisha kwamba ugonjwa umeisha. Vilevile, niendeleo kuwakumbusha watumishi wa afya kote nchini kuendelea kuimarisha afua za kujikinga katika vituo vyote nchini na kuzingatia kanuni za afya za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza (IPC) wakati wote wa kutoa huduma.

**Ndugu Wananchi**, ninawashukuru wataalamu wa afya walio mstari wa mbele na wataalam wengine wakiongozwa na Mganga Mkuu wa Serikali Prof Tumaini Nagu na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera Dr. Issessanda Kaniki kwa kazi nzuri katika kukabaliana na kudhibiti ugonjwa huu. Aidha ninawashukuru Viongozi na Wananchi wote hususani wa Wilaya ya Bukoba na Mkoa wa Kagera kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa serikali katika kukabaliana na ugonjwa huu. Vilevile, ninawashukuru Shirika la Afya Duniani (WHO), UNICEF, US CDC, Africa CDC, USAID, Ireland, MSF na Washirika wengine wa Maendeleo wa Kimataifa na Kitaifa, asasi zisizo za kiserikali na mashirika ya dini kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa kwa Serikali tangu kutangaza mlipuko huu. Ninaomba tuendeleze ushirikiano katika afua za kuzuia, kugundua na kukabaliana na magonjwa ya kuambukiza katika jamii.

**Ndugu Wananchi, Niwahakikishie watanzania na jamii ya Kimataifa kuwa Bukoba ni salama, Kagera ni salama na Tanzania ni salama.** Hivyo, tuendeleo na shughuli na safari zetu bila hofu yoyote. Hata katika Kata za Maruku na Kanyangereko ambapo ugonjwa umeripotiwa sasa hivi kuko shwari, shughuli zote za maendeleo ikiwemo shule, masoko, makanisa na misikiti zinaendelea kama kawaida. Ni matumaini yetu kuwa mlipuko huu ulioathiri sehemu ndogo ya mkoa wa Kagera utaisha ndani ya siku chache kwa kuzingatia Miongozo ya Shirika la Afya Duniani. Kipekee ninapenda kuwashukuru Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani Nchini (WHO) Dkt. Zabuloni Yoti na Mwakilishi mkazi wa UNICEF nchini Bi. Shalini Bahuguna kwa kuambatana nami Wilayani Bukoba na kutembelea kata za Maruku na Kanyangereko na kujiridhisha na hatua zilizochukuliwa katika kudhibiti ugonjwa huu.

Imetolewa na;



**Umyy A. Mwalimu (Mb)**  
**WAZIRI WA AFYA**